# DARUBINI YA DIRA YA MAENDELEO YA TAIFA 2025




Toleo la Kanda ya Kusini

## UTEKELEZAJI WA DIRA YA TAIFA YA MWAKA 2025:KANDA YA KUSINI

### 1. Utangulizi

Toleo hili la Darubini ya Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025 linaelezea utekelezaji wa Dira ya Maendeleo ya Taifa ya mwaka 2025 katika mikoa ya Kanda ya Kusini. Mikoa hiyo ni *Lindi na Mtwara*. Toleo hili litaonesha ni kwa kiasi gani Serikali imetekeleza nguzo zote za Dira 2025 katika Kanda hii. Nguzo hizo ni: (i) Kuboresha hali ya maisha ya Watanzania; (ii) Kuwepo kwa mazingira ya amani,utulivu na umoja; (iii) Kujenga utawala bora na utawala wa sheria; na (iv) Kujenga uchumi imara unaoweza kuhimilina ushindani kutoka nchi nyingine.

### 2. Utekelezaji wa nguzo za Dira 2025

Pamoja na kuelezea hatua mbalimbali zilizochukuliwa na Serikali kutekeleza nguzo za Dira 2025 katika Kanda ya Kusini, sehemu hii inaelezea mafanikio yaliyopatikana na changamoto zilizokuwepo.

### 2.1 Utekelezaji wa nguzo ya kwanza ya Dira 2025

Nguzo ya kwanza ya Dira 2025 ambayo ni Kuboresha hali ya maisha ya Watanzania iliweka malengo kuwa, ifikapo mwaka 2025, Tanzania: (i) iwe na usalama wa chakula; (ii) itoe elimu ya msingi kwa watoto wote; (iii) uwepo usawa wa kijinsia kwenye masuala ya kijamii, kiuchumi na kisiasa; (iv) iwe na huduma bora za afya kwa wananchi wote; (v) itoe huduma bora za afya ya uzazi kwa rika mbalimbali; (vi) ipunguze vifo vya watoto wachanga na vifo vya wanawakevitokanavyo na uzazi; (vii) kuwepo na maji safi na salama; (viii) wastani wa umri wa kuishi uongezeke kufikia kiwango cha nchi za kipato cha kati; na (ix) kuondokana na umaskini uliokithiri. Sehemu hii itaeleza jinsi gani Serikali imetekeleza malengo hayo katika Kanda ya Kusini na changamoto zilizokuwepo.

Katika kuhakikisha uwepo wa usalama wa chakula, Serikali ya Tanzania imekuwa ikigharamia miradi mbalimbali ya kuendeleza kilimo cha umwagiliaji nchini, ili kukuza uzalishaji katika sekta ya kilimo na kuwawezesha wananchi wote kumudu bei za vyakula. Miradi hiyo inatekelezwa kupitia Programu ya Kukuza Maendeleo katika Sekta ya Kilimo Nchini (ASDP[1]), Mpango Kabambe waUmwagiliaji Maji Mashambani (NIMP[2]), Mipango ya Maendeleo ya Kilimo Wilaya (DADPs[3]),Programu Husishi ya Kilimo cha Umwagiliaji Maji Mashambani (PIDP[4])na miradi mingine ya maendeleo ya kilimo kwa kushirikiana na wafadhili wa nchi zilizoendelea. Jedwali lifuatalo linaonnesha baadhi ya skimu na mabwawa ya umwagiliaji yaliyotokana na programu hizo katika mikoa iliyopo Kanda ya Kusini.

---

1 *Agricultural Sector Development Programme*

2 *National Irrigation Master Plan*

3 *District Agricultural Development Programmes*

4 *Participatory Irrigation Development Programme*


**SKIMU NA MABWAWA YA UMWAGILIAJI KANDA YA KUSINI**

| Mkoa | Mabwawa ya umwagiliaji yaliyojengwa | Skimu zilizojengwa/kukarabatiwa |
|---|---|---|
| **MTWARA** | Kitere, Mtwara (hekta 100), Ngongowele (Liwale) | Nangaramo-Masasi; Mpembeli-Mtwara vijijini; Kitere, Mtwara Vijijini(hekta 120); Mahurunga, Mtwara (hekta 500); Kitaya, Mtwara (hekta300); Kitanda, Namtumbo (hekta 100) |
| **LINDI** | Kinyope (hekta 480) Liyuni, Namtumbo (hekta 400) | Makangaga, LindiVijijini (hekta 100), Matekwe Nachingwea; Likunja,Chinokole na Nkowe-Ruangwa |

Serikali vilevile Wizara ya Kilimo na Ushirika imekuwa ikitoa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo ya Kilimo Wilaya ambapo kwa mwaka 2003, mikoa ya kanda ya Pwani ilipokea zaidi ya milioni 100 ili kutekeleza miradi ya kilimo katika vijiji 15 (Mtwara) na Vijiji 12 (Lindi); Likwachu, Chinongwe, Litama na Chiumbati (Nachingwea). Takwimu za Wizara ya Kilimo na Ushirika zinaonesha kuwa miradi ya kuendeleza kilimo cha umwagiliaji katika Kanda ya Kusini imechangia ongezeko la uzalishaji wa mazao ya chakula ambapo mkoani Mtwara, uzalishaji wa mahindi umeongezeka kutoka tani 58,830 mwaka 2005, hadi tani 67,945 mwaka 2011. Vilevile, uzalishaji wa zao la mpunga katika kipindi hicho umeongezeka kutoka tani 19,958,hadi tani 48,281.Pia, katika kuimarisha shughuli za uzalishaji, kuongeza tija na mapato ya wakulima, Serikali ilifanikisha ujenzi wa maghala ya mazao katika vijiji vya Mandawa, Reje, Ndomondo na Mtimbo wilayani Nachingwea, pamoja na vijiji vya Chikundi, Maratani, Maugura, Namajani na Msikisi wilayani Masasi.

Changamoto kuu inayokwaza lengo hili la usalama wa chakula katika Kanda ya Kusini ni utekelezaji hafifu wa miradi mingi ya umwagiliaji, kutokana na kukosekana kwa wataalam wa kutosha kusimamia kwa karibu ujenzi wa miradi hiyo.


Katika kutekeleza Dira 2025, Serikali imeendelea kuhakikisha elimu ya msingi inatolewa kwa watoto wote, ambapo mwaka 2000, Serikali iliondoa ada katika shule za msingi za Serikali ili kila mtoto aweze kupata elimu ya msingi. Katika Mikoa ya Kanda ya Kusini, mafanikio yameonekana ambapo takwimu za Wizara ya Elimu zinaonesha kumekuwa na ongezeko la idadiya watoto wenye umri kati ya miaka 7 hadi 13 wanaosoma katika shule za msingi, kama inavyoonekana katika mchoro ufuatao. Ongezeko hili limechangiwa kwa kiasi kikubwa na uelewa wa kutosha kwa wazazi juu ya umuhimu wa elimu, hasa kwa watoto wa kike.




Changamoto kuu zinazokabili utekelezaji wa lengo hili la utolewaji wa elimu wa msingi ni pamoja na uhaba wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia, uhaba wa nyumba za walimu, uchakavu wa vyumba vya madarasa na uhaba wa vyoo vya kudumu.

Kwa kutambua umuhimu wa usawa wa kijinsia katika kuchochea maendeleo ya kijamii, kiuchumi na kisiasa, Serikali kupitia Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, pamoja na Wizara ya Elimu zimekuwa zikifanya jitihada mbalimbali za kuleta usawa wa kijinsia nchini. Mfano, katika kipindi cha mwaka 2004 hadi 2011, Serikali kupitia Mfuko wa Maendeleo waWanawake,ilitoa mikopo yenye thamani ya shilingi milioni 176 kwa vikundi 335 vya uzalishaji mali vya wanawake mkoani Mtwara. Mikopo hiyo imewanufaisha wanawake kwa kuwawezesha kuendesha shughuli zao za kilimo cha mazao ya biashara na chakula, ufugaji, ushonaji, ususi, kilimo cha mboga, utandaji samaki, mgahawa, mama lishe na biashara ndogo.

Afya bora ni nguzo na raslimali muhimu katika kuchangia maendeleo nchini, hususan katika kuboresha hali ya maisha na kupunguza umaskini. Kwa mantiki hii,Serikali imeongeza ujenzi wa hospitali, zahanati na vituo vya afya katika mikoa iliyopo katika kanda ya Kusini; lengo likiwa ni kurahisisha na kuboresha upatikanaji wa huduma za afya kwa wananchi wote. Takwimu za Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii zinaonesha kuwa hadi mwaka 2013, idadi ya vituo vya Serikali vya kutolea huduma za afya katika mikoa iliyopo Kanda ya Kusini ilikuwa: hospitali 11, zahanati 27 na vituo vya afya 285. Hii imechangiakupunguza vifo vya watoto katika kanda ya Kusini,kama inavyooneshwa kwenye mchoro ufuatao.




Changamoto zilizopo katika utolewaji wa huduma za afya katika mikoa ya Lindi na Mtwara ni upungufu mkubwa wa watumishi wa kada mbalimbali katika hospitali, vituo vya afya na zahanati; kukosekana kwa baadhi ya vifaa-tiba na madawa, kutokana na uhabawa fedha za kununulia madawa kutoka Bohari Kuu ya Madawa ya Serikali (GMS[5]);pamoja na uhaba wa nyumba za watumishi.

Katika kuhakikisha upatikanaji wa maji safi na salama,Serikali imekuwa ikiboresha huduma za maji mijini na vijijini kwa kujenga, kupanua na kukarabati miradi ya maji ya kitaifa. Katika Kanda ya Kusini, miradi mikubwa ya kitaifa ni pamoja na mradi wa Makonde mkoani Mtwara unaohudumia maeneo ya Newala, Tandahimba, vijiji 14 vya Kata ya Nanyamba Mtwara vijijini, Wilaya ya Masasi na Mkoa wa Lindi. Eneo la mradi ni zaidi ya kilometa za mraba 4,020na idadi ya watu wanaohudumiwa na mradi huo ni zaidi ya watu 408,578.Mradi mwingine niwa Masasi-Nachingwea unaotoa huduma ya maji kwa wakazi wa miji hiyo.Mradi huo umewezesha huduma ya maji kuwafikia wakazi 83,128 kati ya wakazi 102,696, sawa na asilimia 81 ya wakazi wote wa mji wa Masasi, wakati kwa mji wa Nachingwea mradi unatoa huduma kwa wakazi 49,471 kati ya wakazi 77,207, ambayo ni sawa na asilimia 64.Vilevile, ili huduma ya maji safi na salama wakazi wa mji wa Lindi na baadhi ya vitongoji vyake, Serikali ilikamilisha

[5] ***G**overnment **M**edical **S**tores*

mradi wa maji wa Ng'apa kwa kuchimba visima 10 kwa ajili ya wakazi 82,000. Changamoto iliyopokwenye usimamizi wa rasilimali za maji nikupungua kwa maji chini ya ardhi, kunakotokana na mabadiliko ya tabia nchi na uharibifu wa mazingira; pamoja na uelewa mdogo wa wananchi katika uhifadhi na ulinzi wa vyanzo vya maji.

Ili kuondoa umaskini uliokithiri kwa wananchi,hususan waliopo vijijini, jitihada zilizofanywa na Serikalini pamoja na kuanzishwa kwa Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini (PSSN[6]) unaotekelezwa na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii TASAF[7] kuanzia mwaka 2000, kwa kushirikiana naBenki ya Dunia. Katika Kanda ya Kusini, mpango huo umekuwa ukitekelezwa katika wilaya 13, ambapo wananchi zaidi ya 83,000 wamenufaika. Pia, Serikali imeimarisha utaratibu wa mauzo ya korosho, ambalo ni zao kuu la biashara katika Kanda ya Kusini, kwa kuanzisha mfumo wa stakabadhi ghalani. Mfumo huu umesaidia wakulima kupata bei nzuri, kutoka shilingi 300 kwa kilo moja ya korosho mwaka 2005/06, hadi shilingi 1,900 kwa kilo mwaka 2010/11, na hivyo kuongeza kipato cha wakulima wa zao hilo.

## 2.2 Utekelezaji wa nguzo ya pili ya Dira 2025

Nguzo ya pili ya Dira 2025 inalenga kuimarisha amani, utulivu na umoja wa nchi, ili kustawisha maendeleo ya kisiasa, kiuchumi na kijamii. Sehemu hii itaeleza jinsi ambavyoSerikali imetekeleza malengo hayo katika Kanda ya Kusinina changamoto zilizokuwepo.

Pamoja na kwamba ni jukumu la kila Mtanzania na kila raia mwema kushiriki kikamilifu kulinda amani na utulivu wa nchi, Serikali imekuwa ikiongoza jitihada hizo kupitiaJeshi la Polisi, ambalo limekuwa likiendeshaoperesheni mbalimbali kukamata wahalifu na kuwafikisha mahakamani.Katika mikoa iliyopo Kanda ya Kusini, Jeshi la Polisi lilifanikiwa kuwakamata zaidi ya wahamiaji haramu 289 mwaka 2007 na kuwafikisha mahakamani. Pia,juhudi za Jeshi la Polisi kulinda amani katika Kanda ya Kusini zilifanikisha kukamatwa kwamaharamia 5 wakiwa na bunduki 5, mabomu 3 na risasi 260 pamoja na meli ya uvuvi waliyokuwa wameiteka kutoka kwa wavuvi wa Sri Lanka mwaka 2012. Watuhumiwa hao waliokamatwa mkoani Lindi walifikishwa mahakamani na kuhukumiwa. Kiujumla, jitihada hizo zimechangia kupungua kwa makosa makubwa ya jinai katika mikoa ya Kanda ya Kusini, kutoka makosa 5,722 mwaka 2008, hadi makosa 2,578 mwaka 2014.

Changamoto kubwa katika usimamizi waulinzi na usalama wa raia na mali zao,ni tatizo la upungufu wa askari Polisi, ikilinganishwa na idadi halisi ya watu wanaohitaji kuhudumiwa katika maeneo husika. Mathalani, uwiano wa kimataifa kwa nchi zilizoendelea ni askari Polisi mmoja kwa watu 250 hadi 350, lakini hapa nchini takwimu za Jeshi la Polisi za mwaka 2014 zinaonesha wastani wa uwiano ni askari Polisi mmoja kwa watu 1,068.

## 2.3 Utekelezaji wa nguzo ya tatu ya Dira 2025

Nguzo ya tatu ya Dira 2025 inalenga kuimarisha utawala bora na utawala wa sheria, kwa kujenga jamii yenye sifa zifuatazo: (i) maadili mema na kuthamini utamaduni; (ii) uadilifu na kuheshimu utawala wa sheria; (iii) isiyokuwa na rushwa na maovu mengine; na (iv) iliyoelimika na inayojiamini, inayojifunza kutokana na uzoefu wake na wa wengine, na yenye kumiliki na kubaini ajenda za maendeleo.

Ili kujenga uadilifu na kuheshimu utawala wa sheria, mnamo mwaka 2007, Serikali ilianzisha Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), ili kuondoa athari za rushwa katika maendeleo ya jamii kiuchumi, kisiasa na kijamii. Taasisi hiyo imekuwa ikifanya tafiti mbalimbali ili kubaini mianya ya rushwa na kuweka mikakati ya kuitokomeza. Katika mkoa wa Lindi TAKUKURU ilifanya udhibiti katika Hospitali ya Mkoa wa Lindi mwaka 2009 kwa kuweka mikakati ya kuziba mianya ya rushwa

---

6 ***P**roductive **S**ocial **S**afety **N**et*

7 ***Ta**nzania **S**ocial **A**ction **F**und*

katika huduma zinazotolewa na hospitali hiyo. Utekelezaji wa mikakati hiyo upo katika hatua inayoridhisha ambapo wastani wa asilimia 72 ya maazimio yametekelezwa.

Katika juhudi zakujenga jamii iliyoelimika, Serikali mnamo mwaka 2009iliamua kutoa kipaumbele kwa wanafunzi wa masomo ya sayansi na ualimu, katika utoaji wa mikopo kwa wanafunzi kutoka Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu, kwa kuwapatia asilimia 100 ya mahitaji ya fedha za mkopo. Lengo lilikuwa ni kuhamasisha wanafunzi wengi kusoma masomo ya sayansi na ualimu, ili kuziba pengo lililopo la wataalamu katika taaluma hizo. Aidha, Serikali kupitia Wizara ya Kilimo na Ushirika imekuwa ikiandaa maonesho ya Nanenane kila mwaka, ili kutoa elimu kwa wakulima, wafugaji, wavuvi na wafugaji nyuki wanaozalisha asali,ili kuongeza tija katika uzalishaji. Katika mwaka 2015, kilele cha maonesho ya Nanenane kilikuwa katika kanda ya Kusini, mkoani Lindi,ambapo kauli mbiu ilikuwa "Matokeo Makubwa Sasa, Tuchague Viongozi Bora kwa Maendeleo ya Kilimo na Ufugaji". Vilevile, Serikali kupitia Wizara ya Kilimona Ushirika, imekuwa ikianzisha mashamba-darasa, ili wakulima waendelee kujifunza mbinu sahihi za kilimo bora kwa vitendo. Mkoani Mtwara, mashamba-darasa yameongezeka kutoka 375 msimu wa 2008/09, hadi 3,105 msimu wa 2010/11 kwenye vitongoji 3,137.

Jitihada nyingine za kujenga jamii iliyoelimika na inayojiamini ni uanzishwaji wa maadhimisho ya Wiki ya Elimu nchini mwaka 2014,chini ya Wizara ya Elimu kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu-TAMISEMI. Lengo la maadhimisho hayo ni kuelimisha umma juu ya umuhimu wa kila mwananchi kuchangia katika kuchochea ari ya kuwa na elimu bora. Jedwali lifuatalo linaonesha idadi ya shule zilizopata tuzo kwa ufaulu mzuri katika kanda ya Kusini. Pia, Serikali imekuwa ikifanya jitihada za kujenga jamii iliyoelimika na inayojiamini, ambapo mwaka 2014 Wizara ya Elimu kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu-TAMISEMI, kwa mara ya kwanza ilianzisha maadhimisho ya Wiki ya Elimu nchini. Lengo la maadhimisho hayo ni kuelimisha umma juu ya umuhimu wa kila mwananchi kuchangia katika juhudi za kuboresha elimu. Jedwali lifuatalo linaonesha idadi ya shule zilizopata tuzo kwa ufaulu mzuri katika Kanda ya Kusini:

**IDADI YA SHULE ZILIZOPATA TUZO KWA UFAULU KANDA YA KUSINI**

| Mkoa | Shule za Msingi | Shule za Sekondari | Jumla |
|---|---|---|---|
| **Lindi** | 146 | 2 | **148** |
| **Mtwara** | 211 | 3 | **214** |

## 2.4 Utekelezaji wa nguzo ya nne ya Dira 2025

Nguzo ya nne ya Dira 2025 inalenga kujenga uchumi imara unaoweza kuhimili ushindani kutoka nchi nyingine. Lengo hilo limepangwa kutimizwa kwa kujenga sekta shindani ya Viwanda, Biashara, Masoko na Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo, ili kujenga uchumi endelevu na kufikia maendeleo ya viwanda kwa kiwango cha kati ifikapo mwaka 2025.

Wizara mojawapo inayohusika katika kutekeleza nguzo ya nne ya Dira 2025 ni Wizara ya Ujenzi kupitia miradi ya ujenzi wa barabara ili kufungua fursa za maendeleo katika maeneo mbalimbali ya nchi, kwani barabara nzuri hurahisisha upatikanaji wa bidhaa na huduma. Katika mikoa iliyopo Kanda ya Kusini, Serikali imefanikisha ujenzi wa barabara zifuatazo kwa kiwango cha lami:

**BARABARA ZILIZOJENGWA KWA KIWANGO CHA LAMI**

| Mkoa | Barabara | Urefu wa barabara (kilometa) | Mwaka wa ujenzi hadi kukamilika |
|---|---|---|---|
| | Mbwemkulu-Mingoyo | 95km | 2003-2008 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| **LINDI** | Nangurukuru- Mbwemkuru | 95km | 2003-2007 |
| | Ndundu-Somanga | 60km | 2013 |
| | Somanga-Masaninga | 33 km | 2001-2005 |
| | Nangurukuru-Lindi | 165 km | 2001-2005 |
| | Lindi-Mingoyo | 25 km | 2001-2005 |
| **MTWARA** | Masasi-Mangaka | 55.1km | 2005-2009 |
| | Daraja la Muungano | | 2005-2009 |

Serikali pia imefanya jitihada ya kuongeza viwanda kwa ajili ya kuongeza thamani ya bidhaa zinazozalishwa Tanzania na kuuzwa nje ya nchi. Serikali kupitia mfuko wa kuendeleza zao la korosho, imetenga shilingi bilioni 2 kwa ajili ya ujenzi wa kiwanda cha kubangua korosho katika Wilaya ya Mtwara,ambapo kiwanda hicho kinatarajiwa kubanguatani 10,000 kwa mwaka. Dhumuni la uanzishwaji wakiwanda hicho ni kuliongezea thamani zao la korosho ili kukuza uchumi wa nchi na kuinua kipato cha wakulima wa zao hilo katika Mikoa ya Kanda ya Kusini.

Jitihada nyingine ni uanzishwaji wa Mamlaka ya Kusimamia Maeneo Huru ya Uzalishaji (EPZA[8])mnamo mwaka 2006,ambapo ndani ya maeneo hayo miundombinu iliyoboreshwa na vivutio hutolewa kwa wawekezaji, kwa lengo la kukuza uwekezaji unaolenga kuimarisha uuzaji bidhaa nje ya nchi na kuongeza Pato ya nchi. Katika Kanda ya Kusini, eneo huru la uwekezaji lenye hekta 2,650 limetengwa mkoani Mtwaranalinajumuisha eneo huru la bandari lenye ukubwa wa hekta 110 kwa ajili ya kuhudumia kampuni zinazowekezakatika shughuli za gesi asilia na mafuta. Uendelezaji wa eneo hilo utawezesha ujenzi wa viwanda na kuibuafursa ya uuzaji wa bidhaa ya gesi ya kupikia na bidhaa nyinginezo zinazotokana na gesi.

[8] ***E**xport**P**rocessing **Z**ones **A**uthority*